

WAMA NAKAYAMA SECONDARY SCHOOL



Katibu Mtendaji,

WAMA – Makao Makuu

S.L.P 10641, Dar es Salaam

Simu ya Ofisi Tel: +255 22 2126516;

Simu : 0713068611

Barua pepe: info@wamafoundation.or.tz / Website: www.wamafoundation.or.tz

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA WASICHANA ZA TAASISI YA WAMA MWAKA 2025

Mzazi/ Mlezi wa: _____

Hongera sana, Mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari ya Wasichana za WAMA ambazo ni Wama Nakayama na Wama Sharaf

Mwanao anatakiwa kuwasili shulenii Jumatatu ya tarehe 13/01/2025 kuanzia saa **2.00 ASUBUHI hadi saa 10.30 JIONI**

KUHUSU SHULE ZA WAMA

Shule ya Sekondari ya Wasichana ya WAMA Nakayama ipo katika mkoa wa Pwani, Wilaya ya Kibiti kijiji cha Nyamisati. Kutoka Dar es Salaam hadi shulenii hapo ni umbali wa Kilomita 162. Shule hii ipo njia kuu ya kwenda Lindi, ukifika eneo liitwalo Bungu ambalo ni kilomita 120 kutoka Dar es salaam, utakuta kibao cha shule upande wa kushoto. Fuata njia hiyo hadi kijiji cha Nyamisati utakuta shule hiyo. Kutoka Bungu hadi Nyamisati ni kilomita 42.

Shule ya sekondari ya wasichana Wama Sharaf ipo katika mkoa wa Lindi .Halmashauri ya Lindi, kijiji cha Mitwero .Kutoka Dar ES Salaam hadi Lindi ni umbali wa kilomita 443.Shule ipo njia kuu ya kwenda Lindi na kutoka na kilomita 7 kutoka Lindi mjini.

Shule hizi zinasomesha wanafunzi wa kike, yatima na walio toka katika mazingira hatarishi. Wanafunzi hawa wanapata udhamini kutoka taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA).

UKARIBISHO NA MAELEKEZO YA MAZINGIRA (ORIENTATION PROGRAM)

Baada ya kuwasili kwa wanafunzi shulenii hapa, kutakuwa na mafunzo ya awali kwa ajili ya kufahamu mazingira vizuri. Mafunzo hayo yatafanyika wiki ya kwanza ya mwaka wa masomo. Lugha kuu shulenii hapa ni Kiingereza mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha ya Kiswahili muda wote anapokuwa shulenii.

VIAMBATANISHO MUHIMU.

Vifuatavyo ni viambatanisho muhimu kwa kila mwanafunzi atakapo ripoti shulenii.

- a) Fomu ya kuchaguliwa kujiunga na shule hii (*barua Hii*)
- b) Fomu ya Uchunguzi wa afya (Medical Examination Form)

Muhimu: Mahitaji yafuatayo yaletwe na mwanafunzi:

1. Mafuta ya kupaka, Sabuni za kuogea na kufulia, Taulo, Mkebe (Mathematical set), Oxford Dictionary, Vitenge 02, Dawa ya meno, Kiwi na Brush, Pads, Chandarua, Ndoo ndogo, Sanduku la bati au la kawaida la ukubwa wa kat, daftari (counter books three quire) 15, jembe na mpini, Mashuka mawili ya pinki, rimu ya karatasi A4, nguo za michezo trucksuit ya rangi nyekundu na raba ya michezo rangi nyeupe
2. Kiatu cheusi cha darasani kisicho na kisigino chenye mkanda mmoja (juma na roza)
3. Juba jeusi kwa ajili ya kushindia kwa wanafunzi waislamu.
4. Sare za shule zitapatikana shulenii hivyo mwanafunzi aje na sare yake aliyokuwa anavaa shule ya msingi

MPANGILIO WA MUHULA WA MASOMO

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza Jumatatu tarehe 13/01/2025

TAARIFA ZA MWANAFUNZI KWA AJILI YA MATUMIZI YA OFISI

Jina kamili _____

- i. Tarehe ya kuzaliwa _____
- ii. Uraia _____
- iii. Kabilia _____
- iv. Dini na dhehebu _____
- v. Jina la shule alikotoka _____
- vi. Mkoala aliomalizia Shule _____
- vii. Mwaka aliomaliza Shule _____
- viii. Namba ya mtihani _____
- ix. Anuani ya mwanafunzi _____

Simu _____ Nukushi_____

Jina la mzazi/mlezi _____

Sahihi ya mzazi /mlezi _____ Tarehe _____

KWA AJILI YA DHARURA

Kama mzazi/ mlezi asipopatikana, Shule itawasiliana na watu wafuatao:

1. Jina _____
Mahusiano-----

Namba ya simu _____

2. Jina _____
Mahusiano-----

Namba ya Simu _____

Mohamed Zome

Afisa Elimu Taasisi ya WAMA

Mawasiliano

Mkuu wa shule

Wama Nakayama

Kibiti – Pwani

0685651449/0687467445

Mkuu wa shule

Wama Sharaf

Mitwero –Lindi

0678578172/07743190741